JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA
BARAZA LA FAMASI

# TAARIFA KWA UMMA

## MAAMUZI YA BARAZA KUHUSU MASHAURI YA UKIUKWAJI WA MIIKO NA MAADILI YA TAALUMA

**DODOMA: JULAI 10, 2026**

Baraza la Famasi ni Taasisi ya Serikali iliyo chini ya Wizara ya Afya iliyopewa jukumu la kusimamia taaluma ya famasi na utendaji kazi wake. Pamoja na majukumu mengine, Baraza lina jukumu la kusimamia na kudhibiti utendaji wa taaluma ya famasi pamoja na maadili ya wanataaluma kupitia kifungu cha. 4 (d – (ii)(iii)(iv)), (f) na 5 (g) cha Sheria ya Famasi, [Sura 311] na Kanuni za Miiko na Mwenendo wa Kitaaluma kwa Wanataaluma wa Kada ya Famasi, 2024.

Ofisi ya Msajili wa Baraza inautaarifu umma kwamba Baraza katika kikao chake cha 60 kilichofanyika tarehe **4 – 5 Juni, 2026,** lilipokea na kujadili mashauri mbalimbali ya uvunjifu wa sheria, kanuni, miiko na maadili yanayoongoza taaluma ya famasi Tanzania Bara yaliyowasilishwa na Kamati ya Nidhamu ya Baraza. Baada ya uchambuzi wa mashauri hayo, ilibainika kuwa wanataaluma husika walijihusisha na makosa mbalimbali, yakiwemo:

1. Kufanya udanganyifu katika utekelezaji wa majukumu ya kitaaluma kwa kuingia makubaliano (mikataba) ya usimamizi na utoaji wa huduma za dawa kinyume na utaratibu.
2. Kutoa huduma zisizoruhusiwa kisheria katika maduka ya dawa, hususani huduma za kitabibu.
3. Kushindwa kutekeleza ipasavyo majukumu ya usimamizi wa famasi.
4. Huduma za dawa kutolewa na watoa huduma ambao hawajasajiliwa na Baraza la Famasi.
5. Kuwasilisha taarifa za udanganyifu kwenye Ofisi ya Msajili kuhusu vigezo vya majengo yaliyokusudiwa kusajiliwa kwa ajili ya utoaji wa huduma za famasi.
6. Kuwasilisha taarifa za udanganyifu kwenye Ofisi ya Msajili kwa lengo la kupata usajili wa awali.

Baada ya kusikiliza mashauri yote, wanataaluma 12 walithibitika kuwa na hatia ya ukiukaji wa sheria, kanuni, miiko na maadili ya kitaaluma na hivyo Baraza limetoa adhabu kama zinavyooneshwa kwenye jedwali hapa chini. Aidha, wanataaluma 2 tuhuma dhidi yao hazikuthibitishwa na Baraza halikuwakuta na hatia.

**ADHABU ZILIZOTOLEWA NA BARAZA NI KAMA IFUATAVYO;**

| NA. | JINA | KADA | ADHABU ALIYOPEWA |
|---|---|---|---|
| 1. | Patrice Paul | Mfamasia | Kusitishiwa jukumu la usimamizi wa famasi kwa muda wa mwaka mmoja kuanzia tarehe 01/7/2026 |
| 2. | Alex H. Mbemba | Mfamasia | Kusitishiwa jukumu la usimamizi wa famasi kwa muda wa mwaka mmoja kuanzia tarehe 01/7/2026 |
| 3. | Fredrick M. Kwandika | Mfamasia | Kusitishiwa leseni ya utendaji wa taaluma kwa muda wa miaka miwili kuanzia tarehe 01/7/2026 |
| 4. | Dawson M. Felician | Mfamasia | Kusitishiwa leseni ya utendaji wa taaluma kwa muda wa mwaka mmoja kuanzia tarehe 01/7/2026 |
| 5. | Kariba Venance | Mfamasia Mtarajali | Kufutiwa usajili wa muda (provisional registration) pamoja na kusitishiwa leseni ya utendaji kama Fundi Dawa Sanifu kwa muda wa mwaka mmoja kuanzia tarehe 01/7/2026 |
| 6. | Joseph C. Dimosso | Fundi Dawa Sanifu | Kusitishiwa leseni ya utendaji wa taaluma kwa muda wa miaka miwili kuanzia tarehe 01/7/2026 |
| 7. | Asteria N. Komba | Mfamasia | Amepewa Onyo |
| 8. | Valentine S. Valentine | Mfamasia | Amepewa Onyo |
| 9. | Mercy Y. Mariki | Mfamasia | Amepewa Onyo |
| 10. | Mercian Majala | Fundi Dawa Sanifu | Amepewa Onyo |
| 11. | Elizabeth Jumanne | Fundi Dawa Sanifu | Amepewa Onyo |
| 12. | Cornelia T. Bayyo | Fundi Dawa Sanifu | Amepewa Onyo |
| 13. | Emmanuel C. Mwera | Mfamasia | Hana hatia |
| 14. | Iddi Hamis Iddi | Fundi Dawa Sanifu | Hana hatia |

Baraza linawakumbusha wanataaluma wote kuzingatia viapo vyao, sheria, kanuni, miiko na maadili ya taaluma ya famasi sambamba na sheria za utumishi wa umma wakati wote wanapowajibika ili kulinda hadhi ya taaluma na kutoa huduma bora kwa wananchi.

Imetolewa na

Boniface Magige
**MSAJILI**
**BARAZA LA FAMASI**